JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# TANGAZO KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs)

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali anayatangazia Mashirika yote Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kwamba yanatakiwa kuwasilisha taarifa za utendaji kazi (***Annual report of activities***) pamoja na taarifa za hesabu za fedha za mwaka zilizokaguliwa (***Annual audited report***) kwa mwaka 2024 pamoja na kulipa ada husika ya mwaka (***Annual subscription fees***) Tshs 50,000/= kwa Mashirika ya Kitaifa (***Local NGOs***) na USD 100 kwa Mashirika ya Kimataifa (***International NGOs***), kama ilivyoainishwa katika **Kifungu cha 29(1)(a)&(b)** cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Sura 56) iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005 na 2019.

Mwisho wa kulipa ada na kuwasilisha taarifa hizo ni tarehe 15.4.2025. Baada ya tarehe hiyo malipo yote ya ada yatalipwa na faini ya Tsh 100,000/= kwa Mashirika ya ngazi ya Kitaifa (Local NGOs) na USD 300 kwa Mashirika ya Kimataifa (International NGOs).

Ulipaji wa Ada na Uwasilishaji wa taarifa kwa mwaka 2024 vifanyike kupitia mfumo wa usajili wa NGOs (***nis.jamii.go.tz***) kwa kutumia akaunti za Mashirika.

Vickness G. Mayao
**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**
19/12/2024
Mawasiliano: 0734986503/0262160250